# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA MBILI

**20 APRILI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA KUMI NA MBILI – TAREHE 20 APRILI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

**128. MHESHIMIWA SHEILA EDWARD LUKUBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Mfereji mkubwa wa kuelekeza Maji Mto Ngerengere ili kunusuru Wakazi wa Kata ya Kihonda na Lukobe kwa mafuriko.

**129. MHESHIMIWA GEORGE VENANCE LUGOMELA (MASWA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara kutoka Senani hadi Gula itakarabatiwa ili iweze kupitika wakati wa masika.

**130. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, upi mkakati kurahisisha upatikanaji mikopo 10% kwa Wanawake wa Vijijini wanaokumbana na changamoto za mfumo wa mtandaoni.

**131. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Soko kubwa la Mazao ya Kilimo Wilaya ya Mkalama kama ilivyoahidi kwenye Ilani.

**132. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (ITWANGI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha Barabara ya lami ya Kahama, Njiapanda ya Lohumbo Mji Mdogo wa Didia.

## OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

### 133. MHESHIMIWA LUCY EDWARD MWAKYEMBE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapa Ajira Vijana wanaojitolea.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

### 134. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, kwa nini Serikali isianzishe eneo mahususi la Viwanda vya kuongeza thamani kwenye mazao ya Misitu litakalohudumia masoko mbalimbali.

### 135. MHESHIMIWA HARAN NYAKISA SANGA (KIGAMBONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, lini Serikali itakuja na mpango wa pamoja ili kutoa suluhu ya mageuzi ya Sekta Binafsi katika kukuza Uchumi.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**136. MHESHIMIWA HAIDERALI HUSSEIN GULAMALI (ILONGERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina Mpango gani wa kutekeleza ahadi ya Ujenzi wa Chuo cha Ufundi VETA Ilongero.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:**

**137. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Wananchi wa Temeke wananufaikaje na uwepo wa Uwanja wa Taifa uliopo Wilayani humo.

**138. MHESHIMIWA EDWARD KISAU OLELEKAITA (KITETO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Iini Mnara wa TBC uliojengwa Kiteto utaanza kufanya kazi.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

## 139. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga uzio wa Uwanja wa Ndege Urambo ili kuutunza vema Uwanja huo na kuwa salama.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

## 140. MHESHIMIWA JOHN JOHN NCHIMBI (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itatoa mikopo nafuu ya Boti za Uvuvi za *Fiber* kwa Wavuvi wa Wilaya ya Nyasa.

## WIZARA YA MAJI:

## 141. MHESHIMIWA DKT. YAHAYA ESMAIL NAWANDA (NEWALA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Mradi wa maji wa Makonde utakamilika.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**142. MHESHIMIWA EDWIN ENOSY SWALLE (LUPEMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Serikali itarejesha Kiwanda cha Chai cha Wakulima wa Chai Lupembe (MUVYULU).

## WIZARA YA UJENZI:

**143. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Kasindaga – Kyebitembe – Karambi hadi Runazi kwa kiwango cha lami.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAENDELEO YA VIJANA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Maendeleo ya Vijana) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**DODOMA**
**20 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**